**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# ANDIKO LA MAPENDEKEZO YA KUREKEBISHA SHERIA YA USHINDANI, 2003 (FAIR COMPETITION ACT, 2003)

**DODOMA** **NOVEMBA, 2021**

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ..... 5
2.0 UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USHINDANI, 2003 NCHINI ..... 7
2.1 SHERIA INAVYOTEKELEZWA ..... 7
2.2 TUME YA USHINDANI ..... 7
2.3 BARAZA LA USHINDANI ..... 9
2.4 BARAZA LA TAIFA LA KUMLINDA MLAJI ..... 10
2.5 UPUNGUFU ULIOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI ..... 10
2.6 HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ..... 16
3.0 HITAJI LA KUREKEBISHA SHERIA YA USHINDANI, 2003 NA ATHARI ZA KUTOREKEBISHWA FCA ..... 16
4.0 UCHAMBUZI KUTOKANA NA UZOEFU WA NCHI NYINGINE ..... 18
5.0 MAMBO MUHIMU YATAKAYOZINGATIWA WAKATI WA KUREKEBISHA SHERIA YA USHINDANI, 2003 ..... 20
5.1 Jina la Sheria na Taasisi ..... 20
5.2 Kuongeza wigo wa tafsiri ya neno Mahakama ..... 20
5.3 Nguvu ya Soko ..... 21
5.4 Washindani kugawana Soko/Wateja ..... 21
5.5 Kuanzisha Leniency Policy ..... 21
5.6 Udhibiti wa Bei ..... 21
5.7 Muungano wa Kampuni ..... 21
5.8 Malalamiko ya Mlaji ..... 22
5.9 Bei za Bidhaa ..... 22
5.10 Utekelezaji wa Maamuzi ya FCC ..... 22
5.11 Kutambua kwa usahihi sheria zote za taasisi za udhibiti ..... 22
5.12 Kuanzisha haki ya rufaa ..... 22
5.13 Mamlaka ya Uteuzi ..... 22
5.14 Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ..... 23
5.15 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji ..... 23
6.0 MATOKEO YANAYOTARAJIWA ENDAPO SHERIA YA USHINDANI, 2003 ITAREKEBISHWA ..... 23

6.1 Sheria Zitakazoguswa na Mapendekezo ya Kurekebisha FCA ........................................... 23
6.2 Matokeo Katika Nyanja Anuai ........................................................................................ 25
7.0 USHIRIKISHWAJI WA WADAU ...................................................................................... 25
8.0 MAHITAJI YA RASILIMALI KATIKA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHINDANI, 2003 ......................................................................................................................... 26
9.0 HITIMISHO ..................................................................................................................... 26

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| EACA | *East African Community Competition Authority* |
| ZCC | Zambia Competition Commission |
| UNCTAD | United Nations Conference of Trade and Development |
| LATRA | Land Transport Regulatory Authority |
| PURA | Petroleum Upstream Regulatory Authority |
| TASAC | Tanzania Shipping Agency Corporation |
| VAT | Value Added Tax |
| NCAC | National Consumers Advocacy Council |
| FCT | Fair Competition Tribunal |
| FCC | Fair Competition Commission |
| SUMATRA | Surface and Marine Transport Regulatory Authority |
| TCAA | Tanzania Civil Aviation Authority |
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| EWURA | Energy, Water and Utilities Regulatory Authority |
| FCA | Fair Competition Act, 2003 |
| SAPs | Structural Adjustment Programs |

## 1.0 UTANGULIZI

Mwanzoni mwa miaka ya themanini, nchi nyingi za Dunia ya Tatu zilianzisha Program ya Mabadiliko ya Kiuchumi (Structural Adjustment Programs – SAPs) ambazo zilisababisha Serikali nyingi kwenye nchi hizo kuingia katika mfumo wa uchumi wa soko (market economy). Pamoja na mambo mengine, Mfumo huo ulielekeza nchi kuachia sekta binafsi kuendesha shughuli za kiuchumi na Serikali kujikita katika kuweka mazingira rafiki na wezeshi ya kukuza shughuli za kiuchumi.

Katika mazingira haya na kwa kuwa nchi yetu siyo kisiwa. Hivyo, Tanzania nayo ilianzisha mfumo wa uendeshaji uchumi kwa njia ya soko mwaka 1986. Aidha, mwanzoni wa miaka ya tisini, Serikali ya Tanzania ilianzisha mageuzi ya mfumo wa Sera na Sheria ili kuendana ya matakwa ya Uchumi wa Soko. Sheria mbalimbali za kipindi cha mfumo wa uchumi hodhi zilifanyiwa marekebisho au kufutwa ili kuendana na matakwa ya nguvu ya soko. Pamoja na mambo mengine, mwaka 1993, mageuzi hayo yalisababisha kufutwa kwa iliyokuwa Sheria ya Udhibiti wa Bei ya Mwaka 1973 (The Price Control Act, 1973) kutokana na kukinzana na misingi ya Uchumi wa Soko. Sheria hiyo ya mfumo wa uchumi hodhi ilikuwa ikizuia ushindani katika soko kwa kupanga bei ya bidhaa na huduma zinazozalishwa au kuagizwa nje na sekta ya umma na binafsi na hivyo kuathiri tija ya soko.

Ili kuendana na misingi ya Uchumi wa Soko, mwaka 1994 Serikali ilitunga Sheria ya Ushindani wa Biashara (The Fair Trade Practices Act, 1994) kwa lengo kuongeza ushindani wa soko kwa kuzuia baadhi ya vitendo ambavyo vingeweza kufifisha ushindani, kudhibiti ukiritimba, hodhi ya nguvu za kiuchumi na bei. Hata hivyo, utekelezaji wake ulikuwa mgumu kutokana na upungufu wa kiuandishi na kiufundi. Upungufu huo ni pamoja na mgawanyo wa majukumu na mpangilio wa kitaasisi uliokuwa kinzani uliosababisha kufutwa kwa sheria hiyo na kutungwa kwa Sheria ya Ushindani, 2003 (Fair Competition Act, 2003 - FCA).

Sheria ya Ushindani, 2003 inalenga kukuza na kulinda ushindani madhubuti kwenye biashara na kumlinda mlaji kutokana na vitendo kandamizi na hadaifu kwenye masoko ya bidhaa na huduma. Aidha, Sheria hiyo ina mamlaka sanjari (concurrent jurisdiction) na taasisi za sekta zinazodhibitiwa ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Energy, Water and Utilities Regulatory Authority - EWURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mawasiliano (Tanzania Communication Regulatory Authority - TCRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Anga (TCAA) na iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA).

Ili kutekeleza malengo hayo, FCA ilianzisha Tume ya Ushindani (Fair Competition Commission - FCC); Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal - FCT); na Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (National Consumers Advocacy Council - NCAC). FCC ina jukumu la kusimamia masuala ya ushindani na kumlinda mlaji, FCT ina jukumu la kusikiliza rufaa zinazotokana na maamuzi ya FCC na taasisi za sekta zinazodhibitiwa ikiwemo EWURA, TCRA, TCAA na iliyokuwa SUMATRA (na sasa LATRA na TASAC). Aidha, NCAC ina jukumu la kutetea maslahi ya walaji kwa kuyawasilisha mbele ya FCC, Serikali na mamlaka za udhibiti pamoja na kuunda Kamati za Walaji za Mikoa na Sekta.

Katika kutekeleza majukumu yake, FCC imefanikiwa kuchunguza na kumaliza mashauri 655 ya kiushindani katika kipindi cha miaka 17 ya utekelezaji wa FCA kama itavoelezewa hapo chini.

Kwa upande wa kumlinda mlaji, FCC imefanyia kazi mikataba ya upande mmoja 744 na kuondoa masharti kandamizi kama vile kubadilisha vigezo na masharti bila idhini ya mlaji na mali ikishauzwa hairudishwi katika mikataba. Aidha, FCC imefanya chunguzi dhidi ya vitendo hadaifu na potofu katika taulo za kike ambapo matokeo ya uchunguzi yalisababisha kurudishwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika taulo hizo mwaka 2019.

Kwa upande wa Baraza la Ushindani, kati ya mwaka 2007 hadi mwaka 2021 imepokea mashauri 374 kutoka kwa FCC na Mamlaka za Udhibiti (EWURA, TCRA, TCAA na iliyokuwa SUMATRA). Kati ya mashauri hayo, 364 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi sawa na ufanisi wa asilimia 97.3. Mashauri hayo yalihusu masuala ya kiushindani kama vile muungano wa makampuni bila taarifa kwa FCC, mienendo baina ya washindani inayofifisha ushindani sokoni; masuala ya kumlinda mlaji ikiwemo kufidia madhara ya huduma zitolewazo chini ya kiwango na kuzuiliwa kupata huduma bila taratibu zinazokubalika; masuala ya udhibiti wa soko kwenye kupanga bei, kusimamia viwango, kusimamia upatikanaji wa huduma bila vikwazo; na masuala ya bidhaa feki kwa uchache tu. Mengi ya maamuzi yaliyotolewa na FCT yameimarisha na kulinda ushindani katika soko kwa kuhakikisha uwajibikaji katika uchumi wa soko hivyo kumnufaisha mlaji, kulete ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa bidhaa/huduma pamoja na usimamizi mzuri wa biashara kwa kuzingatia ubora, vigezo na misingi inayokubalika kitaifa na kimataifa.

Aidha, kwa upande wa Baraza la Taifa la Kumtetea Mlaji – NCAC, Waziri mwenye dhamana ya biashara aliunda Baraza kwa vipindi vitatu tofauti yaani 2005 – 2008, 2008 – 2011 na 2012 – 2015. Katika vipindi tajwa, chini ya Sekretarietiya FCC, NCAC iliweza kuunda kanuni za ndani zilizoweka taratibu za kuajiri Katibu Mtendaji wake. Pia iliunda kamati za kanda (Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za juu Kusini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini) ambazo zilishirikiana nayo katika kupeleka elimu ya mlaji katika maeneo yao ya kiutendaji. Aidha, mchakato wa kuipatia NCAC sub-vote ulianza ili muda wa sekretarieti ya FCC utakapokwisha iweze kusimama yenyewe. Hata hivyo, baada ya kuajiriwa Katibu Mtendaji wa Baraza, mchakato wa haukukamilika na jukumu hilo bado liko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. NCAC ilishindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kukosekana ikama kutokana na kutokuwepo kifungu kinachobainisha uhitaji wa Mkuu wa Sekretarieti na wafanyakazi wengine wa NCAC. Upungufu huu pia ulisababisha NCAC kushindwa kupatiwa sub-vote kwa ajili ya kupatiwa fedha za kuendesha Sekretarieti kama ilitajwa kwenye kifungu cha 93(2) cha Sheria ya Ushindani, 2003.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa FCA, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo zimeathiri utekelezaji wake. Changamoto zinatokana na masuala ya kiuandishi, kisheria na kitaaluma (ushindani na kumlinda mlaji) zinazosababisha ama kushindikana kwa utekelezaji au utekelezaji hafifu wa baadhi ya vifungu vinavyolengwa na mapendekezo ya kurekebisha FCA kama itakavyo wasilishwa

hapa chini. Kutokana na changamoto zilizoathiri utekelezaji, kumekuwa na mapendekezo mbalimbali ya kurekebisha masuala mbalimbali ikiwemo mapendekezo ya kurekebisha Sheria hiyo. Aidha, mapendekezo hayo ya kurekebisha FCA yanafuatia jitihada za Wizara ya Viwanda na Biashara kwenye suala hilo ambapo mwaka 2015 muswada wa marekebisho wa Sheria hiyo ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza kabla ya kuondolewa kwa ajili ya kuboreshwa. Hata hivyo, jitihada za kuwasilisha muswada Bungeni zilikutana na changamoto ya mabadiliko ya Awamu ya Uongozi wa Serikali kufuatia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 na hivyo kuhitaji kuanza mchakato upya ili kujenga uelewa wa pamoja katika ngazi zote Serikalini.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USHINDANI, 2003 NCHINI

### 2.1 SHERIA INAVYOTEKELEZWA

Sheria ya Ushindani, 2003 inatekelezwa kupitia Tume ya Ushindani (FCC), Baraza la Ushindani (FCT) na Baraza la Taifa la Utetelezi wa Mlaji (NCAC). Kupitia Sheria hiyo, taasisi hizo zimepewa majukumu mahsusi ili kuhakikisha malengo ya sheria yanafikiwa.

Sheria ya Ushindani imeipa Tume ya Ushindani jukumu la kuhakikisha ushindani katika masoko ya Tanzania Bara na kumlinda mlaji kwa kuhakikisha muungano wa makampuni unafuata Sheria; Kuchunguza vitendo mbalimbali vinavyokiuka azma ya ushindani na kuchukua hatua za kisheria; kufanya tafiti kuhusu vitendo vinavyofifisha ushindani; na Kufanya uraghibishi (advocacy) kuhusu ushindani.

Kwa upande wa Baraza la Ushindani, FCA imeipa Baraza jukumu la kusikiliza na kutoa uamuzi kuhusu rufani zinawasilishwa kutoka FCC na Mamlaka za udhibiti zinazohusu ushindani na udhibiti wa soko.

Vile vile, Sheria imeipa jukumu Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji jukumu la kuanzisha mabaraza ya kumlinda mlaji ya kimkoa na kisekta na kushauriana nayo, kuwakilisha maslahi ya mlaji mbele ya FCC, Mamlaka za Udhibiti na Wizara za Serikali kwa kuwasilisha maoni, mapendekezo na uzoefu wa utekelezaji bora wa Sheria za Kumlinda Mlaji ulimwenguni. Hata hivyo, NCAC imeshindwa kusimama na kutekeleza majukumu haya kutokana na mapungufu ya kisheria na kibajeti kama ilivyoelezwa awali.

Katika utekelezaji wa Sheria ya Ushindani, 2003, kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kusimamia ukuaji wa uchumi kwa kuhakikisha kuna kuwepo na ushindani katika utoaji huduma na kumlinda mlaji. Pamoja na mambo mengine, Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo yafuatayo.

### 2.2 TUME YA USHINDANI

Tume imefanikiwa kutekeleza majukumu kwa kuwa ni taasisi inayojiendesha (going concern). FCC imeweza kuwa na uongozi wake kwa mujibu wa Sheria ikiwemo Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Bodi ya Taasisi, watumishi na vitendea kazi. Pia FCC ina Ofisi ya Makao Makuu jijini Dodoma na Ofisi Ndogo jijini Dar es Salaam. Kutokana na Sheria hiyo, FCC imeandaa Kanuni na Taratibu mbalimbali za uendeshaji, usimamizi na udhibiti ambazo zinaongoza utendaji wa siku hadi siku wa Taasisi hiyo. Aidha, FCC

huendeshwa kwa vyanzo vya ndani vya mapato na michango ya taasisi za udhibiti zikiwemo TCRA, EWURA, TCAA na iliyokuwa SUMATRA/LATRA. Mwenendo wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na michango ya taasisi kwa miaka mitano (5) iliyopita ni kama ifuatavyo:

***Jedwali Na.1: Mwenendo wa Mapato ya FCC kwa Mwaka 2016-2020***

| VYANZO/MWAKA | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Vyanzo vya Ndani | 5,726,461,036 | 14,836,116,696 | 6,643,084,071 | 9,796,554,661 | 5,818,545,103 |
| Mapato kutoka Taasisi za Udhibiti | 1,392,968,896 | 1,424,137,791 | 1,027,458,564 | 1,164,068,896 | 1,344,068,896 |
| Vyanzo Vingine | 949,084,906 | 382,615,400 | 483,500,895 | 237,330,370 | 224,504,852 |
| JUMLA | 8,068,514,838 | 16,642,869,887 | 8,154,043,530 | 11,197,953,927 | 7,387,118,851 |

Pamoja na majukumu yaliyopo, FCC ilipewa jukumu la kuaianzisha na kuilea katika miaka mitatu ya awali Taasisi ya NCAC ili hatimaye iweze kujiendesha kwa mujibu wa Sheria. Katika kipindii hicho, NCAC ilikuwa ikiendeshwa kwa kutumia fesha na watumishi wa FCC.

Katika utekelezaji wa Sheria ya Ushindani, 2003, kati ya Mwaka 2003 hadi 2021, Tume ya Ushindani (FCC) imefanikiwa kuchunguza na kumaliza mashauri 655 ya kiushindani katika kipindi cha miaka 17 ya utekelezaji wa FCA. FCC imefanya maamuzi ya mashauri kwa kutaja machache suala la makampuni ya ununuzi wa tumbaku yaliyokuwa yanakubaliana wakiwa washindani kufifisha ushindani kwa kuzuia mnunuzi mpya kuingia sokoni mwaka 2020; Uamuzi wa FCC katika shauri hilo uliongeza idadi ya wanunuzi wa tumbaku na hivyo kuongeza ushindani katika soko husika na mkulima kupata bei nzuri.

FCC imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhusu masuala ya kumlinda mlaji. Kati ya Mwaka 2003 hadi 2021, FCC imeshughulikia mikataba 744 ya upande mmoja yenye masharti kandamizi kama vile kubadilisha masharti na vigezo bila idhini ya mlaji. Tume ya Ushindani imewezesha miunganiko ya kampuni (mergers and acquisitions). Mpaka sasa, jumla ya maombi ya muungano wa kampuni 559 yamepokelewa ambapo kati ya maombi hayo, maombi 456 yalipitishwa bila masharti; maombi 60 yalipitishwa kwa masharti; maombi 5 yalikataliwa; maombi 2 yaliondolewa; na maombi 41 uchunguzi unaendelea.

Tume imeendelea kutoa misamaha ya mikataba (exemption to agreements) inayokiuka ushindani lakini yenye maslahi mapana kiuchumi. Tangu Tume ilipoanza kazi zake rasmi, imepokea na kufanyia maamuzi maombi 7 ya misamaha ambapo maombi 5 yalipitishwa kwa masharti, ombi 1 lilipelekwa EWURA na ombi 1 liliondolewa.

Aidha, kati ya Mwaka 2003 hadi 2021, Tume ya Ushindani imesikiliza mashauri 77 yanayohusiana na mienendo inayofifisha ushindani katika masoko na hivyo kukiuka Sheria ya Ushindani kama ifuatavyo: Mashauri 24 yanahusiana na kutokutoa taarifa ya muunganiko wa kampuni (Un-notified mergers); Mashauri 10 yanahusiana na makubaliano yanayokiuka matakwa ya ushindani (anti – competitive agreement); na

Mashauri 5 yanahusiana na makubaliano (*Cartel) chini ya kifungu cha 9 cha sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003.* Mashauri 15 yanayohusiana na Matumizi mabaya ya nguvu ya soko (Abuse of dominant position); na Mashauri 23 yameondolewa na Mlalamikaji yaani Tume;

Kwa upande mwingine, FCC imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu dhana ya ushindani (advocacy). Tume imetoa elimu juu ya sheria ya ushindani kupitia semina na warsha zipatazo 52 kwa wadau mbalimbali wakiwemo Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wa Sera na Mipango, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Wabunge wote, Mahakama, Jumuiya ya Wafanyabiashara na Vyuo vya Elimu ya Juu.

Pamoja na mafanikio hayo, FCC ilikabiliwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo zinazotokana na upungufu wa Sheria kama ilivyofafanuliwa katika sura inayofuata. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa, suluhu kamili ya kurekebisha changamoto hizo ni kuchukua hatua za kurekebisha Sheria husika ili iakisi matakwa ya sasa na yajayo.

## 2.3 BARAZA LA USHINDANI

Baraza la Ushindani – FCT ni taasisi inayojiendesha (going concern) inayotekeleza majukumu yake. Kimuundo, FCT ina uongozi wake kwa mujibu wa Sheria ikiwemo Mtendaji Mkuu anayejulikana kama Msajili wa Baraza anayetekeleza majukumu ya uendeshaji na ya kimahakama. Taasisi pia ina Menejimenti, watumishi wa kada tofauti na vitendea kazi. Kwa ujumla wake FCT ina Baraza linalohudumu kwa "part time" lenye jukumu la kimahakama pekee na watumishi wa kudumu 17. Pia Baraza lina Ofisi Dsm na Ofisi Ndogo Dodoma. FCT ina Kanuni na Taratibu mbalimbali za uendeshaji, usimamizi na udhibiti ambazo zinaongoza utendaji wa siku hadi siku wa Taasisi hiyo. Aidha, FCT huendeshwa kwa vyanzo vya ndani vya mapato na michango ya taasisi za udhibiti zikiwemo EWURA, TCRA, TCAA na iliyokuwa SUMATRA/LATRA. Mwenendo wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na michango ya taasisi kwa miaka mitano (5) iliyopita ni kama ifuatavyo:

***Jedwali Na.1: Mwenendo wa Mapato ya FCT kwa Mwaka 2016-2020***

| VYANZO/MWAKA | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Vyanzo vya Ndani | 2,847,000 | 6,191,000 | 13,887,800 | 20,351,119 | 12,909,254 |
| Mapato kutoka Taasisi za Udhibiti | 943,205,507 | 1,126,588,749 | 1,185,498,203 | 1,317,965,770 | 1,368,875,770 |
| Vyanzo Vingine | 5,817,600 | 3,297,000 | 2,565,000 | 5,003,548 | 12,873,667 |
| JUMLA | 951,870,107 | 1,693,892,247 | 1,136,076,749 | 2,235,027,247 | 1,201,951,003 |

Katika kutekeleza Sheria ya Ushindani, 2003, FCT limeendelea kuhakikisha utekelezaji sahihi wa FCA pamoja na sheria za Mamlaka za Udhibiti (EWURA, TCRA, TCAA, LATRA na PURA) kwa kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya rufaa yanayotokana na maamuzi na amri kutoka FCC na Mamlaka za udhibiti.

Kati ya mwaka 2007 hadi 2021, FCT imepokea jumla ya mashauri 374 kutoka FCC na Mamlaka za Udhibiti. Kati ya mashauri hayo, mashauri 364 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi sawa na ufanisi wa asilimia 97.3. Aidha, kati ya hayo mashauri 89 yalitoka FCC, mashauri 86 kutoka TCRA, mashauri 147 kutoka EWURA, mashauri 16 kutoka iliyokuwa SUMATRA na mashauri 34 kutoka TCAA.

Pamoja na mafanikio hayo, FCT ilikabiliwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo zinazotokana na upungufu wa Sheria kama ilivyofafanuliwa katika sura inayofuata. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa, suluhu kamili ya kurekebisha changamoto hizo ni kuchukua hatua za kurekebisha Sheria husika ili iakisi matakwa ya sasa na yajayo.

## 2.4 BARAZA LA TAIFA LA KUMLINDA MLAJI (NCAC)

NCAC iliundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 92 cha Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 (FCA). Kwa mujibu wa Kifungu cha 93 (2) cha FCA, FCC iliwajibika kutoa Sekretarieti kwa utendaji wa Baraza kwa kipindi cha miaka mitatu. Baada ya hapo, NCAC ilitakiwa kusimama yenyewe katika kutekeleza majukumu yake. Tofauti na FCT na FCC, NCAC ilikabiliwa na changamoto za kimuundo ambapo jitihada za kuweka uongozi wake kwa mujibu wa Sheria ikiwemo Mtendaji Mkuu hazikuwa endelevu.

Kwa miaka mitatu (2007-2010) NCAC iliendeshwa kupitia Sekretariet iliyotolewa na FCC kwa mujibu wa kifugu cha 93(1) cha Sheria ya Ushindani. Aidha, katika kipindi hiki, NCAC ilipata Ofisi zake yenyewe na Katibu wake Mtendaji wa kwanza. Baada ya hapo NCAC kwa kuanzaishwa kwake, inategemewa kuwa Serikali ndiyo ina jukumu la kumlipa mshahara Mtendaji Mkuu na wafanyakazi wengine pamoja na kubeba gharama za shughuli za uendeshaji wa Ofisi.

Jitihada za kuandaa mabadiliko ya Sheria ya Ushindani, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa NCAC ambazo zingeongoza utendaji wa siku hadi siku wa NCAC hazikukamilishwa na hivyo Sekretarieti ya NCAC iliposhindwa kujiendesha ilipata hifadhi ya muda kwenye Ofisi za Wizara ya Viwanda na Biashara Jijini Dar es Salaam na baadae kutoweka.

Hivi sasa jitihada zinafanywa ili kuihuisha upya Sekretarieti ya NCAC na inategemea kuwa na nguvu mpya pindi marekebisho ya Sheria hii yatakapofanywa kwani itaiwezesha kuwa na uwezo wa kujiendesha kwa kuajiri na kuwa na subvote ya kupokea fedha kutoka kweny vyanzo vyake vya fedha ikiwemo mgao kutoka Bunge.

## 2.5 UPUNGUFU ULIOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado kumeendelea kuwepo na upungufu wa kiutendaji na kisheria ambao unasababisha kufifisha ushindani na kumlinda mlaji. Uzoefu wa utekelezaji wa Sheria ya Ushindani, 2003 umekabiliwa na upungufu ufuatao:

### (i) Maudhui ya jina la sheria kutoakisi maudhui halisi ya sheria

Jina la sasa la Sheria na taasisi hayaakisi madhumuni na maudhui ya sheria yenyewe. Maudhui ya jina la sheria na taasisi (Fair Competition) yanazungumzia dhana tofauti na maudhui halisi ya sheria ambayo ni *competition and consumer protection*. Maneno "Fair Competition" yanatambulisha hali ya mshindani kuwa na fursa isiyo ya haki zaidi ya mpinzani wake na hivyo kuuza/kutoa huduma zaidi katika soko. Fursa hizo kwa kutaja chache zinaweza kuwa ukwepaji wa kodi, kuuza/kutoa huduma bandia na kuuza bidhaa/huduma zisizokidhi viwango ambapo masuala hayo hudhibitiwa na sheria nyingine ambazo sio za ushindani. Neno "Competition" linatambulisha maeneo matatu ya kiutendaji ambayo ni: Udhibiti wa mikataba baina ya washindani; Matumizi mabaya ya nguvu ya soko; na Udhibiti miungano ya makampuni/biashara. Ifahamike pia kuwa Sheria ya Ushindani ndio sheria mama ya kumlinda mlaji, suala ambalo haliakisiwi na jina la sheria na Taasisi inayotekeleza sheria husika.

Kutokana na mkanganyiko wa jina la Sheria na jina la Taasisi, kumekuwepo na malalamiko yanayoletwa mbele ya FCC yaliyo nje ya upeo/wigo wa Sheria ya Ushindani. Kwa mfano kuna masuala ya washindani (yasiyo ya ushindani) yanayotokana na Sheria za Kodi, Sheria ya Viwango na Sheria za Biashara za Kimataifa (Anti-dumping). Mkanganyiko huu unasababishwa na tafsiri isiyo sahihi ya neno "*fair competition*" ambapo walalamikaji wanakua na tafsiri pana ambayo inakinzana na mawanda ya sheria. Hii inasababisha mgongano wa tafsiri kati ya Sheria ya Ushindani na Sheria nyingine.

### (ii) Wigo mdogo wa kushughulikia mashauri

FCA imeweka wigo mdogo wa kuwasilisha na kushughulikia mashauri ya utetezi wa mlaji hivyo kuwasababishia wananchi gharama kubwa au kutopata haki kwa haraka. Kwa sasa mashauri madogo madogo ya kumlinda mlaji yanashughulikiwa kuanzia kwenye Mahakama za kawaida ambazo ni gharama na zinachukua muda mrefu kumaliza mashauri madogo madogo.

### (iii) Utambuzi wa uwepo wa nguvu ya soko kutokana na watoa huduma zaidi ya mmoja katika soko

FCA inatambua uwepo wa nguvu ya soko inayotokana na mtoa huduma mmoja pekee (*unilateral conduct*). Katika ulimwengu wa ushindani, nguvu ya soko inaweza kutokana na vitendo vinavyofanywa na watoa huduma zaidi ya mmoja katika soko (*joint dominance*) na hivyo kufifisha ushindani kwa kuongeza bei, kuzuia uwekezaji zaidi katika soko na kupunguza ubora wa bidhaa huku FCC ikishindwa kudhibiti nguvu hizo kutokana na upungufu wa sheria ambapo kwa sasa unadhibiti matumizi mabaya ya nguvu ya soko aliyonayo mtoa huduma au mzalishaji mmoja mmoja. Hili lilikuwa pendekezo namba sita (6) ya mapitio ya sheria ya ushindani yaliyofanywa na UNCTAD (*Voluntary Peer Review of Competition Law and Policy of United Republic of Tanzania) chapisho namba UNCTAD/DITC/CLP/2012/1 la mwaka wa 2012.*

### (iv) Washindani kukubaliana kugawana masoko au wateja

FCA imetoa mwanya kwa washindani kukubaliana kugawana masoko au wateja kinyume na matakwa ya kanuni za ushindani. Kitendo hiki kinaweza kufifisha ushindani kwa njia ya kupanga bei ya bidhaa na huduma hivyo kuongeza gharama za maisha kwa wananchi. Katika ulimwengu wa ushindani kitendo hiki kinatambulika kama kosa la ushindani na hivyo kukatazwa. Mfano katika masoko kama ya uuzaji wa saruji, uuzaji wa vinywaji baridi, uzwaji wa vileo na katika soko la ununuzi wa tumbaku, kampuni hizi zimegawana masoko katika muktadha ambao baadhi ya bidhaa hazipatikani katika masoko mbalimbali ya kijiografia. Ukitazama soda kama *Ginger Ale* au kileo kama *Senator* na *balimi* kinauzwa katika baadhi ya maeneo tu ndani ya nchi. Hali hii inafifisha ushindani, inaongeza bei ya bidhaa na inawapa baadhi ya kampuni nguvu (*dominance*) katika maeneo yao kijiografia. Hali hii hutafsiriwa duniani kote kama mikataba inayofifisha ushindani.

Kwa mfano, kifungu cha 25 (b) cha Sheria ya Ushindani ya Botswana kinakataza washindani kukubaliana kugawana masoko au wateja. Sheria za ushindani marekani, umoja wa ulaya, Kenya na Afrika ya Kusini vilevile ina vifungu vinavyozuia washindani kugawana masoko.

### (v) Kukubaliana bei ya kuuzia bidhaa na huduma

Kwa sasa, mzalishaji (Producer) na msambazaji wa bidhaa na huduma (Distributor) au kati ya msambazaji (Distributor) na muuzaji wa mwisho (retailer) wanaweza kukubaliana bei ya kuuzia bidhaa na huduma kwa rejereja (*Resale Price Maintenance)* na hivyo kuwa na uwezo wa kutoza bei kubwa tofauti na bei halisi na hivyo kuongeza gharama za maisha kwa wananchi. Kwa mfano, makubaliano haya kati ya msambazaji na muuzaji wa mwisho yanaweza tafsiriwa kiushindani **kama upangaji wa bei pale tu kama matokeo ya mpango huo utapelekea bidhaa kuuzwa juu ya bei za kiushindani**. Hili ni kosa la kiushindani dunia nzima. Hali hii imejitokeza katika uuzaji na usambazaji wa vifaa vya ujenzi, vinywaji na bidhaa za viwandani ambazo zinazalishwa na kuuzwa kupitia mnyororo wa wasambazaji. Hatari inayoweza kujitokeza ni madhara kwa mtumiaji wa mwisho kununua bidhaa juu ya bei halisi za kiushindani unaotokana na upangaji huu wa bei unaofanywa na wazalishaji kwenda kwa wasambazaji. Mapendekezo haya yataipa FCA nguvu ya kukataza makosa haya ambayo yapo lakini hayakatazwi kwa sasa na kuleta unafuu wa gharama kwa wananchi.

### (vi) Wigo wa kipimo cha kuzuia maombi ya miungano ya kampuni

Kwa sasa FCA imetoa wigo mdogo wa kipimo kinachotumika kuruhusu au kuzuia maombi ya miungano ya kampuni kupitishwa na FCC ambapo ombi la muungano wa kampuni litakataliwa endopo itabainika kuwa ombi hilo linaimarisha au kutengeneza hodhi ya soko (*"merger is prohibited if it creates or or strengthening of position of dominance in a market").* Kiuhalisia kifungu hiki kinakataza muungano wa makampuni ambapo umiliki wa soko wa kampuni hizi unazidi asilimia 35; na endapo itabainika soko kukosa mshindani thabiti wa kudhibiti matendo yanayowezwa kufanywa na kampuni hizi zinazoungana. Kipimo hiki cha madhara ya muungano wa kampuni ni finyu na hivyo

imesababisha sintofahamu katika nyanja za uwekezaji nchini. Kampuni nyingi zimekua na wasiwasi mkubwa wa kuungana endapo uwezo wao wa kuhodhi soko unavuka 35% kwa pamoja. Katika kuondoa sintofahamu hii katika medani za kiuwekezaji kitaifa na kimataifa, FCC inapendekeza kutanua wigo wa vigezo vya kuzuia muungano wa kampuni zaidi ya vipimo rahisi vya wastani wa 35% ya umiliki wa soko. Vilevile mamlaka zote duniani zinatazama madhara ya miungano ya kampuni kwa kuzingatia kipimo chenye wigo mpana yaani "substantial lessening of competition". **wa hali ya juu kufifisha ushindani** (*merger is prohibited if it **substantially lessens competition**).*

### (vii) Takwa la kutangaza kwa umma miungano wa kampuni

FCA haijaweka takwa la kutangaza kwa umma miungano wa kampuni ili kupata maoni ya umma kuhusu muungano husika. FCC inapokea wastani wa maombi 80 kwa mwaka ambapo wadau mbalimbali Pamoja na walaji huwa wana shauku ya kujua mwenendo wa mashauri haya. Wadau wanaweza kuwa washindani wa kampuni zinazoungana, wasambazaji, mamlaka za Serikali, walaji, wagavi (*suppliers of raw materials*) na wengineo. Wadau hawa ni muhimu na huwa wana athirika na miungano ya kampuni.Uzoefu unaonesha ni muhimu kutangazia umma kuhusu miungano ya kampuni kama ilivyoamuliwa na FCT *katika shauri namba 17 la mwaka 2020 kati ya Medco Energi vs FCC na Moto Mabanga Matiko* ambapo FCT ilikubaliana na uhitaji wa umma kujulishwa kuhusu miungano wa kampuni na kutoa maoni yao.

### (viii) Kifungu kipya juu ya Udhibiti wa Nguvu ya Mnunuzi (Buyer Power Provision)

Sheria ya Ushindani ya sasa haina uwezo wa kushughulika na matatizo ya kiushindani yanayotokana na nguvu aliyonayo mnunuzi (***buyer power/monopsony***). Katika kushughulikia matatizo ya ushindani katika sekta ya kilimo, FCC imebaini kuwa wanunuzi wa bidhaa za kilimo wana nguvu ya soko kuliko wauzaji. Pia aina ya mazao yao yananunuliwa na wanunuzi maalamu na mazao hayo ni ya msimu. Kwa mfano mazao kama tumbaku, korosho, pamba, chai, kahawa yananunuliwa wa wanunuzi wachache wenye nguvu kubwa ya soko. FCA kwa sasa ina uwezo wa kudhibiti nguvu aliyonayo muuzaji (*seller*) na sio mnunuzi. Madhara ya kutokua na kifungu hiki imepelekea FCC kushindwa kusuluhisha kwa ufanisi masuala mtambuka ya kiushindani katika sekta muhimu kama vile bidhaa za kilimo ambazo wanunuzi wana nguvu zaidi ya wauzaji. Hili pia lilikuwa pendekezo namba sita (6) ya mapitio ya sheria ya ushindani yaliyofanywa na UNCTAD (*Voluntary Peer Review of Competition Law and Policy of United Republic of Tanzania) chapisho namba UNCTAD/DITC/CLP/2012/1 la mwaka wa 2012.*

### (ix) Wigo wa FCC kushughulikia mashauri ya mlaji ni mdogo

Wigo wa kushughulikia mashauri ya mlaji kwa mujibu wa FCA ni mdogo kwa kuwa sehemu ya V na VI ya sheria imeelekeza utanzuaji wake ufanywe na mahakama. Hili, limesababisha vitendo hadaifu (*misleading conducts*) na vitendo kandamizi katika soko, ikiwemo vitendo vya uonevu katika makubaliano (*unconscionable conduct*) kuendelea kutamalaki katika soko. Kwa sasa malalamiko yote ya mlaji yanayowasilishwa FCC

hutanzuliwa kwa njia ya maelewano nje ya mahakama (*mediation*). Endapo mtoa huduma/ muuza bidhaa atakataa kutatua lalamiko husika, mlalamikaji hushauriwa kulipeleka mahakamani kama sheria inavyotaka. Marekebisho yanayopendekezwa yatawezesha mashauri madogo madodo kutanzuliwa na ama mahakama au FCC, Pamoja na Mabaraza ya Kata. Aidha, FCC inatekeleza kanuni ya kudhibiti mikataba ya mlaji (Standard Form Consumer Contracts Regulations, 2014), inayoweka utaratibu wa kupitia na kusajili vigezo na masharti ndani ya mikataba hiyo kwa kuondoa vipengere kandamizi na vinavyokwepa uwajibikaji.

**(x) Takwa la watoa huduma kuonesha bei ya bidhaa/huduma**

FCA haijaweka sharti kwa watoa huduma kuonesha bei ya bidhaa/huduma kwa walaji (*price labelling*). Suala hili linaweza kusababisha muuzaji kuuza bidhaa/huduma kwa bei tofauti kwa wateja tofauti tofauti na hivyo kukandamiza wananchi kwa kuwatoza bei kubwa na kuathiri uchumi wao. Mapendekezo ya sheria hii yameainisha hitaji la kuainisha bei ya bidhaa ili kuondoa mkanganyiko na uwezekano wa kumhadaa mteja.kwa hivi sasa hitaji hili la kuonesha bei ya bidhaa si takwa la kisheria kwa mujibu wa FCA.

**(xi) Amri za FCC kutekelezwa kama amri za Mahakama Kuu**

Kwa mujibu wa FCA, amri za FCC zitatekelezwa kama amri za Mahakama Kuu. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa mgumu kutokana na upungufu wa utaratibu wa utendaji kutoelekezwa na FCA. Hali hii inasababisha utekelezaji wa amri za FCA kuwa mgumu na hivyo ama kuchelewesha au kunyima haki kwa wanaopata amri za FCC.

**(xii) Sheria kutotambua baadhi ya taasisi za udhibiti**

FCA inataja sheria za taasisi za udhibiti zenye mamlaka sanjari ya ushindani (concurrent jurisdiction) na FCC ambazo ni sheria zilizoanzisha EWURA, TCAA, TCRA na iliyokuwa SUMATRA. Aidha, FCA imetaja sheria za EWURA na SUMATRA kwa vifupi tofauti na ilivyotaja TCRA na TCAA kwa virefu vyake. Vile vile, marekebisho ya sheria (Petroleum Act, 2015 na SUMATRA) yaliyosababisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA) na Mamlaka ya udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (Land Transport Regulatory Authority – LATRA) na Sheria iliyoanzisha Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation – TASAC); yalitokea baada ya kutungwa kwa FCA mwaka 2003 na kutotambuliwa nayo. Athari mojawapo ya hili ni mgongano na mkwamo wa kisheria katika utekelezaji na utoaji wa maamuzi ya mashauri ya kiushindani katika sekta tajwa.

**(xiii) Haki ya kukata rufaa kwenye mahakama za juu**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki ya msingi ya mtu yeyote kukata rufaa kwenye mahakama za juu pale inapotokea hajaridhika na maamuzi. Kutokana na msingi huo, kwa sasa FCA inatamka kuwa maamuzi ya FCT kuwa ya mwisho na hivyo kutoweka nafasi mtu asiyeridhika na maamuzi yake kukata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa na kusababisha manung'uniko kwa wananchi. Uzoefu wa Baraza la Rufaa za Kodi yaani *Tax Appeals Tribunal* iliyoanzishwa na Sheria ya *Tax Revenue Appeals Act, 2009* unaonesha kuwa maamuzi yake hukatiwa rufaa katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

### (xiv) Mamlaka ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu

Kwa sasa Mkurugenzi Mkuu wa FCC anateuliwa na Mheshimiwa Rais. Ili kuendana na hali ya sasa, mapendekezo ya kurekebisha FCA yanalenga kuihuisha FCA na hali ya sasa;

### (xv) Kutokuwepo kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti

Ikitokea Mwenyekiti wa FCT hayupo kwa sababu yoyote ile, mashauri hayawezi kuendelea. Hali hii imejitokeza mara mbili katika kipindi cha 2004 – 2017 (Aprili 2007 – Aprili 2008 na Mei 2017 – Agosti 2017) na kuathiri usikilizwaji wa mashauri mbele ya FCT. Katika matukio hayo mashauri 16 yalisimama kwa zaidi ya mwaka mmoja na miezi tatu.

### (xvi) Muda wa Wajumbe kwisha pamoja

Wajumbe wa FCT huteuliwa na kumaliza muda wao kwa wakati mmoja na hivyo huathiri usikilizwaji wa mashauri yaliyo mbele ya FCT. Hali hii imejitokeza mara mbili katika kipindi kati ya 2013 na 2021 (Juni 2016 – Agosti 2017 na Agosti 2020 – Juni 2021) na kuathiri usikilizwaji wa mashauri. Katika matukio hayo mashauri 63 yalisimama kwa zaidi ya miaka miwili na hivyo kuleta athari kwa walaji na watoa huduma pale ambapo FCC na mamlaka za udhibiti zilitoa amri ya kusitisha huduma kwa muda, kutoza faini, kulipa fidia kwa mlaji au kufungia mtoa huduma kwa kipindi fulani kwa vigezo mbalimbali na kisha rufaa kutosikilizwa kwa kukosekana Wajumbe mpaka kupelekea muda wa adhabu kuisha au kuteuliwa tena wajumbe baada ya muda mrefu ambapo lengo la uanzishwaji wa FCT kuhakikisha usikilizwaji wa rufaa zinazohusu ushindani na udhibiti wa soko unafanywa kwa haraka halifikiwi.

### (xvii) Malalamiko ya kumlinda mlaji kutosikilizwa

Hali ilivyo sasa, NCAC imeshindwa kuanzisha mabaraza ya kumlinda mlaji ya kimkoa na kisekta, kuwasilisha maslahi ya mlaji mbele ya FCC, Serikali na Mamlaka za Udhibiti na imeshindwa kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kumlinda mlaji. Hali hii imesababisha manung'uniko ya wananchi kuhusiana na malalamiko ya kumlinda mlaji kutosikilizwa na kufikishwa katika mamlaka husika, kuchelewa kwa mashauri ya

kumlinda mlaji kupata ufumbuzi na ustawi wa wananchi kushuka. Changamoto hizo zinasababishwa na NCAC kokosa mamlaka ya kuajiri watumishi kama FCA ilivyotoa mamlaka hayo kwa taasisi dada (FCC kupitia kifungu cha 72 (1) & (2) na FCT kupitia kifungu cha 86) zilizoanzishwa na FCA. Hali hiyo imesababisha NCAC kushindwa kupata ikama na vifungu vya fedha (PE, OC & DEV) na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kama yaliyoainishwa na FCA.

## 2.6 HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Serikali katika azma yake kukuza na kutambua umuhimu wa ushindani na kumlinda mlaji ilichukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zinazofifisha utekelezaji wa Sheria ya Ushindani, 2008. Katika kukabiliana na changamoto hizo hatua zifuatazo zilichukuliwa:

(i) Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Ushindani, 2003 kupitia Sheria ya Fedha, 2020 (Financial Bill, 2020) ambapo kifungu cha 60 (1) kilifutwa maneno “of his annual turnover and not exceeding ten percent of his annual turnover” and kuweka maneno “but not exceeding ten percent of his annual turnover which has a source in Mainland Tanzania”. Aidha, marekebisho mengine yalifanyika kupitia Miscellenious Amendments za Juni, 2021. Marekebisho haya yalilenga kupunguza faini kubwa zilizotafsiriwa kuwa ziliathiri mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

(ii) Zilitengenezwa kanuni (Rules) mwaka 2013 & 2018 ambazo zilitoa miongozo mbalimbali iliyoweza kukabiliana na baadhi ya changamoto kama vile kuweka utaratibu wa namna ya kufanya maridhiano (settlement). Hatua hii ilirahishisha ukamilishaji wa mashauri kwa wakati na kwa gharama ndogo zaidi. na

Kila mwaka, Tume inatoa elimu kwa wadau (kampuni zisizopungua 30 za wanasheria wa kujitegemea) kati ya mwaka 2015-2020 ikielimisha juu ya mambo mbalimbali yenye mkanganyiko au kutoeleweka kama vile maana ya neno ‘*change of control*’ katika muktadha wa ushindani. Aidha, wadau walielimishwa kuwa Tume ina mamlaka juu ya kumlinda mlaji pamoja na kuainisha haki na wajibu wa mlaji. Pia, ilitoa elimu kupitia vyombo vya Habari, semina, warsha na makongamano na ziara za kaguzi kwa makampuni zaidi ya 120 yanayotumia mikataba iliyoandaliwa na upande mmoja juu ya uhitaji wa kusajili mikataba hiyo. Hii imesaidia utekelezaji wa sheria bila shuruti ambapo imepelekea makampuni mengi kuleta mikataba yao ya upande mmoja. Hali hii imepelekea malalamiko yahusuyo mikataba ya mlaji kupungua sokoni.

## 3.0 HITAJI LA KUREKEBISHA SHERIA YA USHINDANI, 2003 NA ATHARI ZA KUTOREKEBISHWA FCA

Sheria ya Ushindani 2003 ni Sheria iliyotekelezwa kwa takriban miaka 18 sasa na kuonesha mafanikio mbalimbali. Pamoja na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa kurerekebisha upungufu uliojitokeza, ni dhahiri kuwa hatua za kutorekebisha Sheria zitaleta athari nyingi kwa taifa kama zilivyobainishwa hapo juu.

## 3.1 Hitaji la Kurekebisha Sheria ya Ushindani, 2003

**Uwepo wa vifungu vinavyokwamisha utekelezaji wa FCA**

Uwepo wa vifungu vinavyokwamisha utekelezaji wa FCA na hivyo kusababisha masoko kutokuwa na hali ya ushindani iliyotazamiwa na mlaji kutolindwa ipasavyo. Athari zinazoweza kujitokeza iwapo mapendekezo ya kurekebisha FCA hayatafanyika hali ya kutokuwepo na ushindani katika masoko na mlaji kutokulindwa itaendelea ambapo bei ya bidhaa na huduma zitaendelea kuwa juu na ubora wa bidhaa/huduma ukiwa hafifu.

Mapendekezo hayo pia, yanatokana na uzoefu wa miaka 17 ya utekelezaji wake kutoka kwa wadau ikiwemo Serikali, Jumuiya ya wafanyabiashara, wanataaluma, taasisi za sekta zinazodhibitiwa, FCC na FCT. Uzoefu huo umepatikana kutokana na muingiliano wa shughuli za wadau kwa mujibu wa FCA, hususan maamuzi ya FCT kwenye mashauri kama vile Tanzania Breweries Limited (TBL) dhidi ya FCC ya mwaka 2010.

## 3.2 Ushauri wa kitafiti

Mwaka 2012 Tanzania ilijitolea kufanyiwa tathmini (voluntary peer review) ya mfumo wake wa ushindani na kumlinda mlaji na Shirika la umoja wa Mataifa la Mkutano wa Biashara na Maendeleo – UNCTAD (***Kiambatisho Na....).*** Tathimini hiyo ilibainisha uhitaji wa FCA kufanyiwa marekebisho yatakayolenga kuboresha ufanisi wa FCC, FCT na NCAC. Baadhi ya mapendekezo ya tathmini ya UNCTAD bado hayajapitwa na wakati miaka 10 baada ya kubainishwa ni pamoja na:

*(i)* ***Uhakika wa vyanzo vya mapato vya Tume na Baraza la Ushindani.***
Sheria ya sasa haitamki wazi suala la ulazima wa Mamlaka za Udhibiti kuchangia bajeti ya Tume na Baraza la ushindani hivyo kusababisha Mapato kutokuwa ya uhakika na ya kutabirika. Hivyo, walishauri kuwa, Sheria ya sasa kuweka sharti ambalo litawataka mamlaka za udhibiti kuchangia bajeti ya Taasisi hizo;

*(ii)* ***Kuhodhi soko kwa pamoja***
Moja ya changamoto kubwa inaathiri utekelezaji wa Sheria ya sasa ni kwamba, FCC haina nguvu ya kisheria inayoweza kuzuia suala la kuwa na nguvu ya soko inayotoka na kuungana kwa pande mbili. Hii inaathiri sana ushindani katika soko na hivyo ripoti hiyo ilishauri kuweka kifungu kinaweka kosa la kuhodhi nguvu ya soko (joint/combined dominance);

*(iii)* ***Mashauri ya Walaji.***
Kwa sasa Tume haina uwezo wa kisheria wa kusikiliza mashauri yanayohusu malalamiko ya walaji. Hivyo, katika kufanya marekebisho sheria itambue mashauri ya walaji na kuyafanyia kazi; na

*(iv)* ***Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa FCT***
FCT inashindwa kutekeleza majukumu pale ambapo Mwenyekiti wa Baraza anapokuwa hayupo kwa sababu yoyote. Upungufu huo wa kiutendaji utatatuliwa kwa kuweka kifungu kipya katika Sheria kinacho tambua nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa FCT.

Uhitaji wa marekebisho ya FCA kama ulivyobainishwa hapo juu uliratibiwa kwa kuandaa rasimu ya andiko na kuwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kukusanya maoni kuhusu marekebisho hayo kama inavyojadiliwa hapa chini.

### 3.2 Athari Zinazoweza Kutokea Iwapo Sheria ya Ushindani, 2003 Haitarekebishwa

(i) Kuendelea kuwepo kwa upotoshaji kwa umma unaotokana na jina la sheria na taasisi zilizoanzishwa chini yake kutoendana na maudhui ya FCA;

(ii) Wananchi wengi kushindwa kutumia fursa ya kupata haki kwenye masuala ya kumlinda mlaji kutoka kwenye vyanzo vilivyo karibu na wanapoishi. Hali hii itaendelea kuwasababishia wananchi gharama, kutopatikana kwa haki kwa haraka na wepesi;

(iii) Kufifia kwa ushindani kwa kuongeza bei, kuzuia uwekezaji zaidi katika soko na kupunguza ubora wa bidhaa kwa kushindwa kudhibiti uwepo wa nguvu ya soko itokanayo na watoa huduma zaidi ya mmoja, upangaji wa bei kati ya mtengezaji na msambazaji na msambazaji na muuzaji wa mwisho na kuendelea kuwepo kwa viasharia vya hatarishi vya ushindani visivyodhibitiwa;

(iv) Kuongezeka kwa vitendo hadaifu na kandamizi kwa walaji kwa kutokuwepo sharti la watoa huduma kuonesha bei ya bidhaa/huduma kwa walaji (price labelling);

(v) Baadhi ya maamuzi ya FCC kutotekelezeka kwa wakati na hivyo kusababisha wananchi kutopata haki yao na Serikali kukosa mapato yake;

(vi) Wananchi kuwa na manunguniko pale wanapohisi kuna uwezekano wa kupata haki kutoka Mahakama ya Rufaa. Hii inatokana na kutokuwepo kwa fursa kwa mtu yeyote ambae hajaridhika na maamuzi ya FCT kukata rufani katika Mahakama ya Rufaa;

(vii) Kutokuwa na chombo cha kupokea, kuchambua na kuwasilisha maoni ya walaji kwa Wizara na FCC na kushauriana kuhusiana masuala ya mlaji kwa pamoja na kukosana kwa mabaraza ya mikoa;

(viii) Kuathiri ustawi wa Watanzania kutokana na uwepo wa mianya ya kufifisha ushindani kwenye masoko kutozibwa dhidi ya vitendo hadaifu na kandamizi kwenye masoko; na

(ix) Kuathirika kwa ufanisi na ubunifu kwenye uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma na hivyo kudhoofisha juhudi za Serikali za kuvutia uwekezaji nchini.

## 4.0 UCHAMBUZI KUTOKANA NA UZOEFU WA NCHI NYINGINE

Nchi nyingine duniani zimeweka mfumo maalum wa kushughulikia masuala ya ushindani na kumlinda mlaji. Nchi hizo zimeanzisha taasisi mahsusi za kiutendaji kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki na mlaji analindwa dhidi ya vitendo

hadaifu katika masoko. Aidha, nchi hzo zimekuwa na Sheria zenye vipengele au marekebisho yanayoakisi maono yetu ya sasa kuhusu mahitaji ya kurekebisha Sheria hii. Uzoefu wa nchi hizo ni kama ifuatavyo:

### 4.1 Jamhuri ya Zambia

Mageuzi ya kiuchumi nchini Zambia yalisababisha kutungwa kwa Sheria iliyojulikana kama *The Competition and Fair Trading Act, 1994*. Sheria hiyo ilianzisha Tume ya Ushindani ya Zambia (Zambia Competition Commission - ZCC) ambayo ilianza kufanya kazi mwaka 1997.

Utekelezaji wa sheria hiyo ulikumbwa na matatizo na mkwamo ikiwemo tafsiri ya neno 'concerted practice' na 'vertical restraints', tafsiri ya neno 'merger' na taratibu za kutoa taarifa za 'merger', masuala ya maslahi ya umma na ratiba ya utoaji maamuzi ya mashauri. Masuala ya ujumla yaliyoleta mkwamo wa utekelezaji wa sheria hiyo yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Kutokuwa na nguvu ya kutosha kufanya upelelezi (Limited investigative powers);

(ii) Kutokuwa na nafuu/adhabu za kiutawala za kutosha (Limited administrative remedies);

(iii) Kutokuwepo kwa utaratibu wa kutoa nafuu ya adhabu kwa wakosaji wanaojisalimisha (Absence of a leniency programme);

(iv) Kutokuwepo kwa uratibu mzuri wa kisheria wa namna ya kushughulikia muingiliano wa shughuli za Tume ya Ushindani na Mahakama na Tume ya Ushindani na taasisi za udhibiti; na

(v) Kutokuwepo kwa sheria moja inayosimamia masuala ya kumlinda mlaji hivyo kufanya utekelezaji wa vifungu vinavyohusu kumlinda mlaji kuwa mgumu.

Upungufu huo ulisababisha kutungwa kwa sheria mpya iitwayo *Competition and Consumer Protection Act, 2010* ambayo pamoja na kurekebisha upungufu uliotajwa hapo juu, ilifuta sheria ya awali ya mwaka 1994. Kutokana na marekebisho hayo, Zambia imepata mafanikio hasa katika eneo la kumlinda mlaji ambapo mashauri yameongezeka zaidi ya mara 10 ya mashauri ya awali na maombi ya watuhumiwa kupitia *leniency program* ambapo mashauri zaidi ya 30 ambayo yasingegunduliwa sasa yameshughulikiwa kwa ufanisi.

### 4.2 Jamhuri ya Botswana

Botswana ilitunga Sheria ya Ushindani mwaka 2010 (The Competition Act of 2010) iliyoanzisha Tume ya Ushindani na Mamlaka ya Ushindani za Botswana kwa ajili ya kushughulikia masuala ya kiushindani kwenye miungano ya kampuni, matumizi mabaya soko na masuala mengine ya ushindani. Baada ya utekelezaji kwa miaka sita, kulionekana kuwepo na upungufu uliosababisha kurekebisha sheria. Mapungufu hayo ni pamoja na masuala ya kumlinda mlaji ma yale ya ushindani kushughulikiwa na taasisi tofauti.

Mapungufu hayo yalisababisha utekelezaji wa sheria yao kuwa mgumu na hivyo kusababisha kufanya marekebisho. Mwaka 2017, Bunge la Jamhuri ya Botswana lilipitisha marekebisho hayo na kubadilisha jina la tume na kuitwa *Competition and Consumer Authority*. Aidha, maboresho hayo yaliweka majukumu ya kumlinda mlaji chini ya Competition and Consumer Authority yaliyokuwa chini ya Wizara husika.

**Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitunga Sheria yake ya ushindani yaani *The East African Community Competiton Act of 2006* ambayo ilianzisha *East African Community Competition Authority* (EACA). Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho kwa mara ya kwanza mwaka 2010 ili kutambua ongezeko la nchi wanachama kutoka nchi 3 mpaka nchi 5. Mwaka 2021, sheria hiyo imefanyiwa tena marekebisho ili kuoanisha vifungu vinavyodhibiti masuala ya muungano wa kampuni (mergers) na uzoefu wa kimataifa, kuipatia EACA hadhi ya utu wa kisheria (legal personality), kuiwezesha EACA kutoa adhabu za kifedha na kukusanya fedha zinazotokana na adhabu.

Kutokana na uzoefu wa nchi za Zambia na Botswana na ule wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mamlaka hizo zimefanya maboresho ya sheria zao kwa kufuta ama kurekebisha baadhi ya vifungu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sheria za ushindani. Mapitio ya uzoefu wa mamlaka zingine kama ulivyochambuliwa hapo juu unaonesha kuwa uzoefu wa Tanzania unaendana kwa kiasi kikubwa na uzoefu wa nchi ya Zambia. Aidha, uzoefu wa Botswana na ule wa Jumuiya ya Afrika Mashariki una baadhi ya masuala ambayo yanaendana na mapendekezo ya kurekebisha FCA na hivyo kuwa wa manufaa kwa Tanzania.

## 5.0 MAMBO MUHIMU YATAKAYOZINGATIWA WAKATI WA KUREKEBISHA SHERIA YA USHINDANI, 2003

Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria ya Ushindani tunapendekeza masuala muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kuboresha Sheria hiyo kama yalivyofafanuliwa kwenye bangokitita **(Kiambatisho Na….):**

### 5.1 Jina la Sheria na Taasisi

Inapendekezwa kubadili jina la sheria na taasisi ili kuakisi maudhui halisi ya FCA. Mabadiliko yanayopendekezwa ni pamoja na kubadili jina la sheria kuwa *Competition and Consumer Protection Act* na kubadili majina ya taasisi kuwa *Competition and Consumer Protection Commission* na *Competition Appeals Tribunal;*

### 5.2 Kuongeza wigo wa tafsiri ya neno Mahakama

Marekebisho ya sheria yatawezesha mabaraza ya kata kuwa na nguvu ya kisheria ya kushughulikia mashauri ya madogo madogo ya kumlinda mlaji na hivyo kupanua wigo wa upatikanaji wa haki kwa urahisi, kupunguza gharama na muda wa kupata haki kwa wananchi.

### 5.3 Nguvu ya Soko

Marekebisho ya Sheria hiyo yatatambua uwepo wa nguvu ya soko itokanayo na watoa huduma zaidi ya mmoja ili kuweza kudhibiti hali hiyo inapojitokeza katika masoko na kubainisha mienendo inayotambulika kama matumizi mabaya ya nguvu ya soko. Marekebisho haya yanalenga kutamka na kutoa tafsiri ya mienendo inayotambulika kama matumizi mabaya ya nguvu ya soko ili kuzuia makosa ambayo kwa sasa yapo na hayakatazwi na FCA;

### 5.4 Washindani kugawana Soko/Wateja

Marekebisho ya Sheria yatatambua dhana ya kugawana soko/wateja kama kosa kwa kuwa vitendo hivyo kufifisha ushindani kwa kuathiri bei ya bidhaa na huduma. Mapendekezo ya marekebisho haya yatawezesha kuzuia makosa kama haya ambayo kwa sasa yanafanyika lakini hayakatazwi na FCA.

### 5.5 Kuanzisha Leniency Policy

Marekebisho ya Sheria yatatoa mwanya kwa washiriki wa uvunjaji wa sheria wa masuala ya ushindani kujisalimisha kwa FCC kwa kutoa taarifa kuisaidia FCC kufanikisha uchunguzi na kupata nafuu ya adhabu kwa kuanzisha dhana *Leniency policy kama* ijulikanayo kwenye ulimwengu wa masuala ya ushindani;

### 5.6 Udhibiti wa Bei

Kukataza udhibiti wa bei ya kuuzia kwa rejereja (Resale Price Maintenance) kati ya mtengenezaji (Producer) na msambazaji (Distributor) au kati ya msambazaji (Distributor) na muuzaji wa mwisho (retailer) ili kuzuia madhara ya kupanga bei baina ya washindani;

### 5.7 Muungano wa Kampuni

Sheria itaongeza wigo wa masuala yanayoweza kuzuia maombi ya muungano wa kampuni kupitishwa na FCC kwa kubadili zuio kutoka “creation or strengthening of position of dominance in a market” na kuwa “substantial lessening of competition”. Aidha, Sheria itaongeza muda wa awali wa kukamilisha uchambuzi wa ombi la muunganiko wa kampuni na kutoa uamuzi kutoka siku 14 hadi 30 ili kuendana na uzoefu uliopatikana katika muda wa miaka 17 ya utekelezaji;

### 5.8 Malalamiko ya Mlaji

Marekebisho ya Sheria yataipa FCC mamlaka ya kushughulikia baadhi ya malalamiko ya mlaji ikiwemo kwa kutaja machache vitendo hadaifu dhidi ya mlaji (unconscionable conduct) na masuala ya fidia kwa hasara itokanayo kwa kuvunjwa aina fulani za mikataba (breach of implied conditions in consumer contract) ambayo yanashughulikiwa na Mahakama peke yake;

### 5.9 Bei za Bidhaa

Mapendekezo ya kurekebisha sheria yataweka sharti kwa muuzaji kuonesha bei ya bidhaa/huduma inapooneshwa kwa lengo la kuuzwa na kuhakikisha wananchi wanalipa bei shindani kwa bidhaa na huduma hivyo kukuza ustawi wa mwananchi mmoja mmoja na uchumi kwa ujumla hususan wa viwanda.

### 5.10 Utekelezaji wa Maamuzi ya FCC

Marekebisho ya Sheria yataweka utaratibu wa namna ya utekelezaji wa maamuzi ya FCC kama amri za Mahakama Kuu ili wananchi waweze kufaidi utekelezaji wa maauzi kwa haraka zaidi;

### 5.11 Kutambua kwa usahihi sheria zote za taasisi za udhibiti

Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria yatazitambua Sheria zote za Mamlaka za Udhibiti kwa usahihi ambazo zina mamlaka sanjari (concurrent jurisdiction) na FCA. Sheria hiyo ni pamoja na Sheria zilizoanzisha EWURA, TCAA, TCRA, PURA, LATRA;

### 5.12 Kuanzisha haki ya rufaa

Marekebisho ya Sheria yatatoa haki ya kwenda Mahakama ya Rufaa kwa mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa FCT ili kupunguza manung'uniko kwa wananchi;

### 5.13 Mamlaka ya Uteuzi

Kwa sasa Mkurugenzi Mkuu wa FCC anateuliwa na Mheshimiwa Rais. Ili kuendana na hali ya sasa, mapendekezo ya kurekebisha FCA yanalenga kuihuisha FCA na hali ya sasa kwa kumtamka Mheshimiwa Rais kama mamlaka ya uteuzi ya Mkurugenzi Mkuu wa FCC;

### 5.14 Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe

Mapendekezo yataweka utaratibu wa Mheshimiwa Rais kuteua kwa vipindi vinavyopishana (staggering) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wenye sifa za ama Jaji wa Mahakama Kuu au Jaji wa Mahakama Kuu mstaafu kuhudumu kwenye FCT. Aidha, Kuweka utaratibu wa Mheshimiwa Rais kuteua wajumbe wa FCT kwa vipindi vinavyopishana (staggering of tenure) ili kuhakikisha muendelezo wa usikilizwaji wa mashauri yaliyopo mbele ya FCT kwa wakati wote na kujenga kumbukumbu ya taasisi; na

### 5.15 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji

Kuipa NCAC uwezo wa kuajiri kwa kuweka uhitaji wa kuajiri watumishi na kuweza kupokea fedha kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ikiwemo mgao kupitia bajeti inayopitishwa na Bunge kwa mujibu wa FCA.

## 6.0 MATOKEO YANAYOTARAJIWA ENDAPO SHERIA YA USHINDANI, 2003 ITAREKEBISHWA

### 6.1 Sheria Zitakazoguswa na Mapendekezo ya Kurekebisha FCA

Mapendekezo ya Marekebisho ya FCA yatagusa sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2003 (Tanzania Communications Regulatory Authority, 2003) itaguswa katika vifungu vya 3, 17 (4),19 (2) (a), 41 (1) na 41 (2) (b) ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 3 ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 3, 35 (2), 36 (3) na 42 (2) ili kubadilisha jina la Baraza la Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal;

(ii) Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985 (Ward Tribunals Act, 1985) kuongeza kifungu kinachoipa nguvu ya kisheria (jurisdiction) ya kushughulikia mashauri madogo madogo (small claims) yanayohusu kumlinda mlaji;

(iii) Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ya mwaka 2001 (Energy and Water Utilities Regulatory Authority, 2001) itaguswa katika vifungu vya 3 (c), 18 (4), 20 (2) (a), 38, 38 (1) na 38 (2) (a) ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 3 ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 3(c), 28(2), 29, 29(1), 29(3), 36, 36(2), 36(3), 36(4) na 36(5) ili kubadilisha jina la Baraza la

Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal;

(iv) Sheria ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga (Civil Aviation Act, 2001) itaguswa katika vifungu vya 2(1)(c), 44(4), 46(2)(a), 63(1) na 63(2)(a) ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 2(1)(c) na 46(2)(a) ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 2(1)(c), 44(6), 54(2), 55(1), 55(3) na 61(2) ili kubadilisha jina la Baraza la Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal;

(v) Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu ya mwaka 2019 (The Land Transport Regulatory Authority Act, 2019) itaguswa katika vifungu vya 3, 20(2)(a) na 28(1) ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 3 ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 3, 28(1), na 33(6) ili kubadilisha jina la Baraza la Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal;

(vi) Sheria ya Wakala wa Usafirishaji wa Majini Tanzania ya mwaka 2017 (Tanzania Shipping Agencies Act, 2017) itaingiza vifungu vitakavyo itambua jina jipya la sheria ya Competition and Consumer Protection Act, majina mapya ya Taasisi za Competition and Consumer Protection Commission na Competition Appeals Tribunal;

(vii) Sheria ya Mafuta ya Petroli ya mwaka 2015 (The Petroleum Act, 2015) itaguswa katika vifungu vya 166, 183(1), 183(2) na 255 ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 183(3) ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 244, 247(3) na 255 ili kubadilisha jina la Baraza la Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal; na

(viii) Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta ya mwaka 2010 itaguswa katika vifungu vya 3 na 184 ili kubadilisha jina la sheria kutoka Fair Competition Act, 2003 na kuwa Competition and Consumer Protection Act, kifungu 3 ili kubadilisha jina Tume ya Ushindani kutoka Fair Competition Commission na kuwa Competition and Consumer Protection Commission na vifungu 3 na 40(2) ili kubadilisha jina la Baraza la Ushindani kutoka Fair Competition Tribunal na kuwa Competition Appeals Tribunal.

## 6.2 Matokeo Katika Nyanja Anuai

Katika mapendekezo ya kurekebisha FCA nyanja mbalimbali zitaguswa kama ifuatavyo:

(i) Jina la sheria na taasisi zilizoanzishwa chini yake kuendana na maudhui ya sheria hivyo kuwezesha wananchi kufaidika zaidi na uwepo wa sheria hii na kuondoa uwezekano wa upotoshaji kwa umma;

(ii) Wananchi wengi kupata fursa haki kwenye masuala ya kumlinda mlaji kwa karibu zaidi na gharama nafuu kupitia Mabaraza ya Kata yaliyopo kila kata nchi nzima;

(iii) Ongezeko la ushindani kwenye masoko utakaosababisha upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa bei nafuu, kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa watanzania:

(iv) Kuongezeka kwa wepesi wa upatikanaji wa haki ya kumlinda mlaji kwenye masuala kama *unconscionable conduct* na *breach of implied conditions in consumer contract* kwa kuruhusu FCC kushughulikia masuala hayo;

(v) Kumalizika na/au Kupungua kwa vitendo hadaifu na kandamizi kwa walaji kupitia sharti la watoa huduma kuonesha bei ya bidhaa/huduma kwa walaji (display of price);

(vi) Kutekelezeka kwa amri za FCC kwa haraka;

(vii) Kumuwezesha mtu yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi ya FCT kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa;

(viii) Uendelevu wa wa kusikilizwa kwa mashauri yaliyowasilishwa FCT muda wote na hivyo kuwezesha kupatikana kwa haki haraka;

(ix) Kuiwezesha NCAC kufanya jukumu lake la kukusanya kuchambua, kushauriana na kuwasilisha maoni ya walaji kwa Wizara na FCC;

(x) Kuongeza ustawi wa watanzania kwa kuongeza ushindani unasababisha uchumi imara, uhakika wa ajira na vipato vya wananchi kuongezeka; na

(xi) Kuongezeka kwa ufanisi na ubunifu kwenye uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma na hivyo kuvutia uwekezaji nchini.

## 7.0 USHIRIKISHWAJI WA WADAU

Zoezi la utekelezaji wa Sheria na pia uibuaji na kufanya mapendekezo ya kurekebisha Sheria hii ni zoezi shirikishi. Bainisha ushiriki wa wadau (umma na binafsi) katika kuibua upungufu unaopendekezwa na pia kupendekeza hatua za kuchukuliwa.

Rasimu ya Andiko la Mapendekezo ya kurekebisha FCA liliwasilishwa kwa Wadau katika vikao vilivyofanyika tarehe 7 Februari, 2020 na 12 Februari, 2020 jijini Dodoma na Dar es Salaam mtawalia kwa lengo la kupata maoni ili kuweza kuboresha rasimu ya andiko. Mihutasari ya vikao hivyo vimeambatishwa kama **Kiambatisho Na.....** na **Kiambatisho Na.....** na kuwa sehemu ya andiko hili. Aidha, kuna wadau walishiriki na kutoa maoni yao kwa njia ya maandishi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.....**. Wadau hao walionesha matumani mapya na kuunga mkono mapendekezo hayo kwani yataleta matokeo chanya kwa sasa na siku zijazo kwa maufaa mapana ya nchi.

## 8.0 MAHITAJI YA RASILIMALI KATIKA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHINDANI, 2003

Mchakato wa mawasilisho haya ulianza mwaka ... na ulihusisha wadau katika ngazi na hatua mbalimbali ambazo zimegharimu fedha na kutumia watu mbalimbali. Katika kukamilisha zoezi la marekebisho ya sheria, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, FCC na FCT itatumia rasimaliwatu wa ndani ya Serikali na fedha katika kukamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria hii hadi hatua ya kuanza utekelezaji wake. Katika maandalizi ya awali ya marekebisho ya FCA, Shilingi 60,000,000 zimeshatumika.

Ili kamilisha hatua zilizobaki, kiasi cha Shilingi milioni mia moja na arobaini (TZS 140,000,000) zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Kiasi hicho kinajumuisha gharama za kukamilisha andiko, waraka kuhusiana na mapendekezo ya kurekebisha FCA, gharama za mikutano ya wadau pamoja na gharama za kuchapisha sheria yenyewe, kuisambaza na kuelimisha umma.

Aidha, inatarajiwa kuwa mapendekezo ya kurekebisha FCA yatawasilishwa katika mamlaka ya maamuzi kuanzia ngazi ya *Cabinet Secretariat* kabla ya mwisho wa mwezi Novemba, 2021 ili maamuzi ya Baraza la Mawaziri yaweze kufanyika mapema na ikiwezekana kabla ya mwisho wa mwezi Desemba, 2021.

Muswada wa mapendekezo ya kurekebisha FCA utawasilishwa na kujadiliwa katika mkutano wa mwezi Januari, 2022 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Elimu kwa umma itatolewa kuanzia mwezi Februari 2022 na sheria kuanza kutumika kuanzia mwezi Aprili, 2022.

## 9.0 HITIMISHO

Umuhimu wa kurekebisha Sheria ya Ushindani, 2003 umeonekana bayana katika maelezo yaliyotangulia. Hii ni pamoja na kutatua changamoto za kuandishi na Kitaaluma (Ushindani na Kumlinda Mlaji) ambazo zimesababisha kwa namna moja au nyingine kufifisha ushindani na kumlinda mlaji. Aidha, kurekebishwa kwa Sheria ya Ushindani, 2003 kutakidhi hoja za za wadau nchini ambao kwa ujumla waliweka msisitizo na kuednelea kuishauri Serikali kuhusu marekebisho hayo.

Mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Ushindani, 2003 ni muhimu katika kuhakikisha ustawi wa uchumi wa viwanda nchini. Utekelezaji wa maboresho yanayopendekezwa utasaidia kukuza ubunifu katika masoko, kukuza ustawi wa uchumi wa wananchi kwa

kutumia bidhaa/huduma zenye kiwango cha juu na zinazopatikana kwa bei nafuu na shindani. Pia, utekelezaji wa Sheria hii utasaidia kuongeza ajira kwa watanzania na kukuza uchumi nchini.

**************